# Uchunguzi wa Sababu za Mtumizi ya Lakabu za Wanafunzi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni Nchini Tanzania

*Joyce Henock Nyiti*[1] na *Adventina Buberwa*[2]
[1]*Idara ya Elimu Sekondari Meru*
[2]*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Miongoni mwa maeneo ambayo lakabu hutumika ni katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu matumizi ya lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn na kubainisha sababu mbalimbali za kutumia lakabu katika ufundishaji wa lugha kwa ujumla. Licha ya kubainisha sababu hizo, tafiti hizo ziliangazia lugha mbalimbali bila kuangazia sababu za matumizi ya lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn mahususi. Makala haya yameshughulikia sababu za matumizi ya lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka kwa walimu 6 wanaofundisha Kiswahili kama Lgn na wanafunzi 15 kutoka katika vyuo/taasisi 03 nchini Tanzania ambazo ni Taasisi ya Kiswahili na Utamaduni (KIU), Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC) na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA). Data zimekusanywa kwa mbinu ya usaili na kuwasilishwa kimaudhui kisha zikatolewa maelezo yaliyoongozwa na Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C. Gardner, 2005. Sababu zilizobainika katika matokeo hayo ni pamoja na kuwapa wanafunzi utambulisho, kupata urahisi wa kuwakumbuka wanafunzi kwa lakabu zao, kuchochea motisha ya wanafunzi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn, kurahisisha ufundishaji wa sarufi, kukidhi kipengele cha kiutamaduni, kuepuka makosa ya matamshi ya majina ya wanafunzi na kutumia lakabu kwa sababu tu ni utaratibu wa chuo/taasisi husika. Makala haya yanapendekeza kuwapa walimu mafunzo kuhusu matumizi ya lakabu ili watambue faida zake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Pia, wito unatolewa na makala haya kwa wataalamu wengine kuchunguza madhara ya kutumia lakabu zisizofaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ili waweke bayana maarifa hayo.**

**Maneno Muhimu:** *Sababu, Lakabu za Wanafunzi, Lugha ya Kigeni, Ufundishaji na Jifunzaji*

**Utangulizi**

Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni (kuanzia sasa Lgn) nchini Tanzania ulianza kabla ya miaka ya 1960 wakati wakoloni wakijifunza lugha hiyo kwa sababu ya kuwasiliana na wafanyakazi wa Kitanzania katika shughuli mbalimbali zilizohusishwa na ukoloni. Aidha, kwenye miaka ya 1967 serikali ya Tanzania ilianza kupokea wataalamu wa kujitolea kutoka nchi kama Denmaki ili kufanya kazi za kimaendeleo. Kutokana na hali hiyo, mafunzo ya lugha ya Kiswahili yalianza kutolewa nchini Tanzania ili wafanyakazi hao waweze kukamilisha kazi za kimaendeleo zilizokusudiwa. Kuanzia miaka ya 1980 kulikuwa na makundi ya wanafunzi wa vyuo vikuu waliofika Tanzania kutoka mataifa kama Denmaki, Marekani, Ufini, Ujerumani, na Uingereza. Makundi hayo yalifika Tanzania kujifunza Kiswahili kama Lgn kutokana na kuanzishwa kwa programu mbalimbali za ufadhili wa wanafunzi wa vyuo vikuu ili wakajifunze Kiswahili ng'ambo na kukamilisha masomo yao ya shahada mbalimbali (Wa'Njogu, 2008). Ili kutimiza mahitaji ya wanafunzi hao, mbinu mbalimbali za ufundishaji wa Lgn zimekuwa zikitumika. Sambamba na matumizi ya mbinu hizo lakabu nazo zimekuwa zikitumika katika ufundishaji wa lugha ya kigeni licha ya kutokutambulika kuwa miongoni mwa vipengele vya mbinu za ufundishaji wa lugha ya kigeni.

Zaidi ya hayo, tafiti zimefanyika kuhusu matumizi ya lakabu kwa ujumla katika maeneo ya kitaaluma kama vyuo vikuu na shule za sekondari na kubainisha sababu za kutumia lakabu katika

maeneo hayo. Tafiti zilizofanywa na Mapunda (2014), Sobane (2016) na Mensah na Ndimele (2020) zimeonesha kuwa baadhi ya lakabu hutolewa na wanafunzi kwa wahadhiri kwa sababu ya kuakisi sifa na tabia mbaya za wahadhiri kama vile kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wa kike, kutokuwa na maarifa yanayotosha katika masomo wanayofundisha na kuakisi sifa ya uvivu. Pia, baadhi ya lakabu hutumiwa kuonesha sifa na tabia nzuri za wahadhiri kama vile kuwa na maarifa ya kutosha wakati wa kufundisha somo au mada fulani. Kwa upande wa lakabu za wanafunzi, katika vyuo vikuu tafiti zimefanywa na Kuranchie (2012), Filani na Melefa (2014) na Koehn, (2015. Katika shule za sekondari lakabu za wanafunzi zimeshughulikiwa na Atolagbe (2015), Jamalvandi na Jamalvandi (2016), Starks, na Taylor-Leech (2021). Tafiti hizo kwa pamoja zimeonesha kuwa kwa asilimia kubwa wanafunzi hupewa lakabu kwa sababu ya kuakisi maumbile, sifa zao kama vile uwezo wao wa kitaaluma na tabia zao. Pamoja na tafiti hizo kubainisha sababu za kitaaluma sababu hizo hazikuhusishwa na ujifunzaji wa Lgn.

Tafiti zilizochunguza matumizi ya lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn ni pamoja na tafiti za Diao (2014), Bobrova, (2022) na Xinran (2023). Tafiti hizo zimebainisha sababu mbalimbali za kutumia lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn. Sababu zilizobainishwa ni kurahisisha ujifunzaji wa lugha ya kigeni na kukumbuka majina ya wanafunzi (Diao, 2014) na kutaka wanafunzi wafanikiwe kujifunza lugha ya kigeni (Bobrova, 2022). Pia, sababu nyingine ni kuwapa wanafunzi utambulisho unaotokana na lugha nyingi za kigeni pamoja na kupata historia za maisha ya wanafunzi (Xinran (2023). Aidha, kuna changamoto zinazotokana na matumizi ya lakabu katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni kama vile baadhi ya wanafunzi kushindwa kupata umilisi wa lugha ya kigeni (Bobrova, 2022).

Pamoja na umuhimu na changamoto zilizotokana na matumizi ya lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn katika tafiti tangulizi, tafiti hizo hazikuchunguza sababu za kutumia lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni mahususi. Kwa kuwa wanafunzi wa kigeni hufika Tanzania kujifunza Kiswahili kama Lgn na baadhi yao huwa na lakabu huku wengine wakipewa au kujipa lakabu baada ya kufika Tanzania katika taasisi au vyuo vinavyofundisha Kiswahili kama Lgn, watafiti wamepata raghba ya kuchunguza sababu za matumizi ya lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa mbinu ya mahojiano kutoka kwa walimu 6 wanaofundisha Kiswahili kwa wageni na wanafunzi 15 waliojifunza Kiswahili kama Lgn katika vyuo/taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Pia utafiti huu ulihusisha vyuo/taasisi tatu zinazofundisha Kiswahili kwa wageni nchini Tanzania. Vyuo/taasisi hizo ni Taasisi ya Utamaduni na Kiswahili (KIU), Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC) na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA). Walimu walipatikana kwa mbinu ya usampulishaji nasibu ambapo kwa kila chuo/taasisi mtafiti aliandaa karatasi na kuweka kwenye boksi. Miongoni mwake karatasi mbili ziiliandikwa alama ya ndiyo, kwa hiyo mwalimu aliyeokota karatasi iliyoandikwa ndiyo alishiriki katika utafiti. Aidha, mbinu ya usampulishaji nasibu na si nasibu zilitumika kuwapata wanafunzi walioshiriki katika utafiti. Kwa upande wa usampulishaji si nasibu mtafiti alitumia usampulishaji lengwa kuwahusisha wanafunzi wote waliokuwa na lakabu katika utafiti kisha baadaye alichgua sampuli ya kushiriki katika utafiti. Ili kupata sampuli hiyo, mtafiti aliweka karatasi kwenye boksi na miongoni mwake karatasi tano ziliandikwa alama ya ndiyo. Kwa hiyo, mwanafunzi aliyeokota karatasi iliyoandikwa alama ya ndiyo alipata nafasi ya kushiriki kwenye utafiti. Kwa upande mwingine vyuo/taasisi zilizohusishwa kwenye utafiti zilipatikana kwa mbinu ya usampulishaji lengwa. Data zimekusanywa kwa mbinu ya usaili na kuwasilishwa kwa mbinu ya kimaudhui. Kwa kila maudhui yalitolewa maelezo yaliyoongozwa na Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C. Gardner (2005). Makala haya yamegawanyika katika vipengele vitano ambavyo ni ikisiri, utangulizi, ufafanuzi wa modeli iliyoongoza uchanganuzi wa data, sababu za matumizi ya lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn na hitimisho.

**Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C, Gardner (2005)**

Kutokana na kubainika kuwa lakabu zinatumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn ilionekana kuwa Modeli ya Elimu ya Kijamii (kuanzia sasa MEK) ya Robert C. Gardner (2005)

inafaa kuongoza uchanganuzi wa data za makala haya. Modeli hiyo inatokana na Nadharia ya Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni ya Robert C. Gardner ambayo aliianzisha mwishoni mwa 1959 na mwanzoni mwa 1960. Nadharia hiyo inaonesha umuhimu wa mtazamo kuhusu mazingira ya ujifunzaji na kazi ya motisha katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Aidha, 1975 Gardner na Smythe walianzisha MEK ikiwa ni sehemu kubwa ya nadharia hiyo ikimakinikia matazamo kuhusu mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya pili/lugha ya kigeni. MEK imepitia maboresho katika vipindi mbalimbali ambavyo vilishughulikiwa na wataalamu kama vile, Gardner (1985), Gardner na Maclntyre (1993), Gardner (2000) na Gardner (2005). Lengo la kuiboresha modeli hiyo ni kuondoa utata wa baadhi ya vipengele, kuongeza, kupunguza na kuunganisha baadhi ya vipengele ili kuhakikisha kuwa modeli hiyo inatosheleza mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni.

Modeli ya Elimu ya Kijamii imeonekana kuwa ni muhimu kuongoza uchanganuzi wa data za makala haya kwa sababu modeli hii inasisitiza kuwa mafanikio ya ujifunzaji wa lugha ya pili/kigeni yanatokana na motisha ya ujifunzaji. Anafafanua kuwa motisha ya ujifunzaji hutokana na mtazamo wa mjifunzaji kuhusu mazingira ya ujifunzaji, mwingiliano wa tamaduni na matarajio ya mjifunzaji ya kuitumia lugha ya pili/kigeni anayojifunza. Kwa pamoja, vipengele hivyo vinawapa wajifunzaji mafanikio kama havikuwapa hofu ya ujifunzaji. Lakini, kama vipengele hivyo vitawapa wajifunzaji hofu ya kujifunza watapata mafanikio ya kiwango cha chini katika ujifunzaji wa lugha lengwa. Modeli hiyo imeteuliwa kutumika katika makala haya kwa sababu vipengele vinavyojenga motisha ya ujifunzaji vina uhusiano na matumizi ya lakabu katika ufundishaji na ujifuzaji wa Kiswahili kama Lgn. Hivyo basi, MEK imetumika katika uchanganuzi wa data kwa kuchunguza kama matumizi ya lakabu ni sehemu ya mojisha ya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama Lgn au la!.

**Matumizi ya Lakabu katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni Nchini Tanzania**

Uzoefu unaonesha kuwa ni utaratibu wa kawaida kwa vyuo/taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania kutumia lakabu za wanafunzi kwa kipindi cha ujifunzaji ilhali wana majina yao halisi. Usaili uliofanywa kwa wanafunzi na walimu ulibainisha lakabu 94 ambazo wanafunzi walitumia wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn katika vituo vya KIU, MS TCDC na SUZA. Wanafunzi hao ni wale waliojifunza Kiswahili katika vyuo/taasisi hizo kuanzia mwaka 2016 mpaka mwaka 2021. Lakabu hizo zimeaonesha kuwa zimeundwa na aina mbalimbali za majina kama vile majina ya watu, majina ya wanyama, majina ya ndege, majina ya mimea, majina ya madini kama almasi na dhahabu, majina ya kawaida na vifupisho vya majina ya wanafunzi. Aidha, lugha zilizotumika katika uteuzi wake zinahusisha lugha za wenyeji ambazo ni Kiswahili, Kimeru, Kimasai na Kizanaki ambazo ni asilimia 96.808. Pia, lugha za kigeni kama Kiingereza na Kijerumani zimehusika katika uteuzi wa lakabu za wanafunzi kwa wa asilimia 3.191. Baada ya uchanganuzi wa data iliyopatikana imebainika pia kuwa baadhi ya wanafunzi hupewa lakabu kabla ya kufika katika vyuo/taasisi zinazofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania huku wengine wakipewa lakabu hizo baada ya kufika katika vyuo na taasisi husika.

**Sababu za Matumizi ya Lakabu za Wanafunzi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn Nchini Tanzania**

Watoataarifa waliotoa taarifa zilizokamilisha makala haya walithibitisha kuwa zipo sababu za kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania. Taarifa hizo zilipatikana kutoka kwa 6 wanaofundisha Kiswahili kama Lgn nchini Tanzania na wanafunzi 15 waliojifunza Kiswahili katika vyuo na taasisi zilizobainishwa awali katika makala haya. Sababu zilizobainishwa na watoataarifa hao zimefafanuliwa kama ifuatavyo;

**Kuwapa Wanafunzi Utambulisho**

Mtu yeyote katika jamii asipokuwa na jina linalomtambulisha huweza kuathirika kisaikolojia kwa sababu utambulisho wa mtu ni muhimu kama utamaduni wake (Agyekum, 2006). Kwa hiyo, suala la kuwapa wanafunzi wa kigeni lakabu ni la muhimu kwa sababu linawafanya watambulike na kukubalika katika jamii wanayojifunza lugha yake. Katika kubainisha sababu za kuwapa wanafunzi lakabu baadhi ya walimu walieleza kuwa huwapa wanafunzi lakabu kwa sababu wanafunzi wakiwa

na majina ya wenyeji ni rahisi kutambulika na kukubalika kwa wenyeji. Aidha, walimu hao walieleza kuwa kutambulika na kukubalika kwa wanafunzi na wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili kunawafanya wanafunzi wafanikiwe kujifunza lugha hiyo kirahisi kutokana na kushirikishwa katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano mwalimu mmoja anaeleza:

> … jamii ya wenyeji ikisikia majina kama Amani, Malaika, Mashaka, Waridi na Tausi hata itatambua kuwa haya ni majina ya Waswahili, hivyo jamii inamwomona kuwa ni mwenzao na watampa ushirikiano pale unapohitajika.

Matokeo haya yanaungwa mkono na Modeli ya Elimu Kijamii ya Robert C. Gardner (2005) ambayo inaeleza kuwa mjifunzaji wa lugha ya kigeni mwenye sifa za utamaduni wa jamii yenye lugha lengwa hupata urahisi wa kuchangamana na jamii hiyo. Aidha, hali hiyo ya kuchangamana na wazungumzaji wazawa wa lugha ya kigeni hurahisisha ujifunzaji wa lugha hiyo.

Pia, matokeo hayo yanaonesha kuwa wanafunzi wanapotambulika kwa lakabu zao hupata urahisi wa kujifunza Kiswahili na utamaduni wake kwa sababu ya mwingiliano kati yao na wazungumzaji wazawa wa Kiswahili. Nukuu ifuatayo inadhihirisha hali hiyo:

> …..ninawapa wanafunzi lakabu kwa sababu zinawasaidia kujifunza Kiswahili na utamaduni wake kutokana na kupata fursa ya kujichanganya na jamii ya wazawa.

Kama inavyoonekana katika nukuu hiyo, lakabu za wanafunzi zinatumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa sababu kupitia lakabu hizo wanafunzi wanapata fursa ya kujichanganya na wazungumzaji wazawa wa Kiswahili jambo ambalo huwarahisishia ujifunzaji wa Kiswahili na utamaduni wake.

Suala la kuchangamana na wazungumzaji wazawa wa lugha ya kigeni limeelezwa katika Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C, Gardner (2005) kuwa hurahisisha ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa sababu wajifunzaji wa lugha ya kigeni wanapojichanganya na wazungumzaji wazawa wa lugha lengwa hushiriki katika shughuli mbalimbali zinazotumia lugha hiyo. Pia, modeli hiyo imesisitiza kuwa moja ya sifa za walimu wanaofundisha lugha ya kigeni ni kuwa na uwezo wa kumudu ufundishaji wa lugha ya kigeni. Kwa hiyo, walimu wa namna hiyo ni wabunifu wa kutumia mitindo mipya ya kurahisisha ufundishaji wa lugha lengwa (Oxford, 2003; Saleh, 2019). Kutokana na maelezo hayo walimu wanaotumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn sit u wanawapa wanafunzi utambulisho bali ni wabunifu kwa sababu wanatumia mtindo au mkakati unaowasaidia wanafunzi kuchangamana na wazawa wa lugha ya Kiswahili.

**Kuwakumbuka Wanafunzi kwa Majina**

Wataalamu kama Kennedy na Zamuner (2006) wanaeleza kuwa lakabu ni miongoni mwa zana zinazosaidia kuwakumbuka na kuwatofautisha watu katika makundi mbalimbali. Baadhi ya walimu walioshiriki katika utafiti huu walieleza kuwa hutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn kwa sababu zinarahisisha kuwakumbuka wanafunzi. Baadhi yao waliongeza kuwa majina ya wanafunzi wa kigeni ni magumu hivyo ni vigumu pia kuyakumbuka. Kwa hiyo, wanapotumia lakabu za wanafunzi zinazotokana na majina ya wenyeji inakuwa rahisi kwao kuzikumbuka lakabu hizo kwa sababu ni majina waliyoyazoea katika jamii zao. Naye, mtoataarifa mwingine ambaye ni mwalimu alieleza kuwa, mwalimu anapokumbuka majina ya wanafunzi wakati wa ufundishaji wanafunzi hao huelewa kirahisi kwa sababu wanamfurahia mwalimu na somo analofundisha. Matokeo hayo ni sawa na maelezo ya Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C. Gardner (2005) ambayo inaeleza kuwa mwalimu anayefundisha lugha ya kigeni ana nafasi ya kuwatengenezea wanafunzi mazingira mazuri ya ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Maelezo hayo yanakubaliana na matokeo yaliyobainika katika sehemu kwa sababu suala la kuwakumbuka wanafunzi wanafunzi kwa majina limebainika kuwa linawafanya wafurahie mazingira ya ujifunzaji. Maelezo hayo hayatofautiani na maelezo ya Glenz, (2014) ambaye anaeleza kuwa kuwakumbuka wanafunzi kwa majina yao kuna faida nyingi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa sababu wanafunzi hujihisi kutambulika na kuheshimiwa. Pia, anaongeza kuwa kuwakumbuka wanafunzi, hurahisisha ushirikishwaji wa wanafunzi wakimya katika somo. Ingawa Glenz hakuzungumzia ufundishaji na

ujifunzaji wa lugha ya kigeni lakini maelezo yake yanaongeza msisitizo kuhusu umuhimu wa walimu kuwakumbuka wanafunzi kwa majina yao wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa hiyo, kwa mujibu wa maelezo hayo, walimu wanapotumia lakabu za wanafunzi na kuweza kuwakumbuka kwa majina hayo wanawatengenezea wanafunzi mazingira mazuri ya ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

**Motisha ya Wanafunzi ya Kujifunza Kiswahili kama Lgn**

Ili ujifunzaji uwe na mafanikio unahitaji motisha. Kauli hiyo inaungwa mkono na wataalamu mbalimbali (Yule, 2010; Koehn, 2015; Saleh, 2019) ambao wanathibitisha kuwa, lakabu zina zinachochea motisha katika ujifunzaji. Yule (2010) anaongeza kuwa moja ya sababu zinazomfanya mjifunzaji kujifunza lugha ya kigeni/pili ni motisha. Naye Saleh (2019) anasisitiza kuwa motisha kwa wajifunzaji wa lugha ya kigeni ni muhimu kwa sababu huwasababishia mafanikio katika ujifunzaji wa lugha lengwa. Maelezo ya wataalamu hao kwa pamoja yamedhihirishwa na matokeo ya utafiti huu baada ya mahojiano na walimu walioshiriki katika utafiti huu. Miongoni mwao baadhi walieleza kuwa hutumia lakabu za wanafunzi kwa sababu huchochea motisha ya ujifunzaji. Walimu hao walieleza kuwa wakati wa ujifunzaji wanafunzi wengi hupenda kuwa na majina ya wenyeji ama ya Kiswahili au ya asili. Kwa hiyo, wanafunzi wanapopewa lakabu hizo huzitumia kama kichocheo cha motisha ya ujifunzaji. Baadhi ya lakabu zilizobainishwa na watoataarifa kuwa zinazotumika kuchochea motisha ya ujifunzaji ni kama zinavyoonekana katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali Lenye Mifano ya Lakabu Zilizotumiwa Kuwa Motisha Wanafunzi Kujifunza Kiswahili**

| Na. | Lakabu | Lugha | Sababu |
|---|---|---|---|
| 01. | Almasi | Kiswahili | Alikuwa na kasi kubwa wa kujifunza Kiswahili. |
| 02. | Jasusi | Kiswahili | Alitarajia kufanya kazi ya ujasusi. |
| 03. | Kamusi | Kiswahili | Alitaka kufahamu kila neno la Kiswahili. |
| 04. | Mirisho | Kimeru | Alipewa jina la asili la baba wa familia aliyoishi nayo kwa sababu alipenda sana kujifunza Kimeru na Kiswahili kwa pamoja. |
| 05. | Mlowezi | Kiswahili | Alikuwa anatarajia kurudi kuishi Tanzania akachagua jina hilo baada ya kufahamu maana yake. |
| 06. | N'kanfu | Kimeru | Alipewa jina hilo katika familia ya Wameru aliyoishi nayo kwa sababu yeye ni mtoto wa tatu wa kike katika familia yao na mtoto wa tatu wa kike kwa Wameru anaitwa *N'kanfu.* |
| 07. | Nyerere | Kizanaki | Alitarajia kuwa mhamasishaji wa matumizi ya Kiswahili chuoni kwake kama Rais *Nyerere* alivyofanya kwa Watanzania. |
| 08. | Sanaipei | Kimasai | Alipewa jina hilo na familia ya Kimasai ambayo aliishi nayo kujifunza lugha ya Kiswahili na utamaduni wake kwa sababu alikuwa mrembo. Kwa kawaida Wamasai humwita msichana mrembo *Sanaipei*. |
| 09. | Simba | Kiswahili | Alijipa lakabu hiyo kwa sababu alikuwa na matarajio ya kujifunza Kiswahili na kufanya kazi kwa malengo kama simba anavyowinda kwa malengo. |
| 10. | Tamasha | Kiswahili | Alipenda kushiriki kwenye matamasha ya Kiswahili. |
| 11. | Tuzo | Kiswahili | Alifanya matendo mazuri kama kuwasaidia wanafunzi waliokuwa na changamoto za ujifunzaji akaambiwa anastahili kupewa tuzo. |
| 12. | Upendo | Kiswahili | Alipewa jina hilo kwa sababu aliwasaidia wanafunzi wenzake walipohitaji msaada wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili. |
| 13. | Zawadi | Kiswahili | Alikuwa na uwezo mkubwa wa kujifunza Kiswahili. |
| 14. | Zuena | Kiswahili | Alipenda muziki wa Kiswahili uitwao 'Zuena Mtoto aliyeumbika'. |

Sambamba na mifano iliyobainishwa katika jedwali hilo hapo juu, watoataarifa wawili ambao ni walimu walieleza kuwa baadhi ya wanafunzi hupewa lakabu kabla ya kufika Tanzania zikihusishwa na motisha ya ujifunzaji. Kwa hiyo, baada ya wanafunzi kufika Tanzania, walimu huendelea kuzitumia lakabu hizo, hali hiyo inadhihirisha kuwa lakabu za wanafunzi hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn kwa sababu ya kuchochea motisha ya wanafunzi ya ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Aidha, kutokana na usaili uliofanyika matokeo mengine yameonesha kuwa baadhi ya walimu huenda mbele zaidi na kutumia lakabu za wanafunzi kwa namna ya kuchochea motisha ya ujifunzaji. Kwa mfano wakati wa usaili mtoataarifa mmoja ambaye ni mwalimu alitoa

mfano wa majibizano kati yake na mwanafunzi ambayo aliyafanya ili kuchochea motisha ya wanafunzi katika ujifunzaji. Majibizano hayo ni kama ifuatavyo:

> **Mwalimu**: 'wewe Simba unafanya nini darasani wakati simba wenzako wanawinda porini?
> **Mwanafunzi**: ninawinda Kiswahili.

Majibizano hayo yanadhihirisha kuwa baadhi ya walimu hutumia lakabu za wanafunzi kwa lengo la kuchochea motisha ya ujifunzaji.

Matokeo hayo yanakubaliana na maelezo ya Modeli ya Elimu ya Kijamii ya Robert C. Gardner (2005) ambayo yameonesha kuwa moja ya mambo yanayojenga motisha ya mjifunzaji ni mikakati ya ujifunzaji. Kulingana na matokeo yaliyobainika suala la baadhi ya walimu la kutumia lakabu za wanafunzi kuchochea motisha ya ujifunzaji linaashiria kuwa baadhi ya lakabu za wanafunzi ni kichocheo cha motisha ya ujifunzaji. Kwa mujibu wa Reyes na Rodriguez (2006) matumizi ya mikakati kama sehemu ya kuchochea motisha ya ujifunzaji ni ya muhimu kwa sababu wanafunzi wanaojifunza Lgn wanatofautiana umahiri na mbinu za kujifunzaia . Hivyo basi, suala hilo lina tija katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lgn kwa sababu ni mbinu inayoweza kuwasaidia wanafunzi wengi kufanikiwa kujifunza lugha ya kigeni licha ya tofauti zao.

**Kurahisisha Ufundishaji wa Sarufi**

Sababu nyingine iliyobainika baada ya kuchunguza data zilizokusanywa ni kurahisisha ufundishaji wa sarufi ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Maelezo ya walimu 3 miongoni mwa waliohojiwa yalionesha kuwa lakabu hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa sababu ni mbinu inayorahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Watoataarifa hao walieleza kuwa kwa upande wao hutumia lakabu kama mbinu ya kufundishaia sarufi. Mtoataarifa mmoja alieleza kuwa yeye huonesha viambishi vinavyounda lakabu na kufafanua kazi zake. Aidha, watoataarifa wengine wawili walieleza kuwa wao huwapa wanafunzi kazi za kuandika kuhusu historia za lakabu zao na kuziwasilisha darasani. Wakati wa uwasilishaji walimu hao hunukuu makosa ya kisarufi na sarufi mpya inayojitokeza kisha baada ya uwasilishaji au siku inayofuata hufundisha sarufi iliyokosewa na sarufi mpya iliyojitokeza wakati wa uwasilishaji wa kazi za wanafunzi.

Pia, watoataarifa hao walieleza kuwa sababu nyingine ya kutumia lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn ni kwamba baadhi ya wanafunzi hutumia lakabu kama mkakakti wa kujifunzia. Hali hiyo inathibitishwa na maelezo ya Oxford (2003) kuwa mitindo mipya inayotumiwa katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni hukuza tabia ambazo hurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Kukubaliana kwa matokeo ya utafiti huu na maelezo ya Oxford kunadhihirisha kuwa upo umuhimu wa kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn kwa sababu zinakuza tabia za ujifunzaji zinazorahisisha ujifunzaji wa Lgn.

**Kukidhi Kipengele cha Utamaduni**

Utamaduni ni miongoni mwa vipengele ambavyo haviwezi kutengenishwa na ujifunzaji wa lugha kwa sababu lugha na utamaduni ni kama pande mbili za sarafu (Reyes na Rodriguez (2006);Yi, 2010; Atolagbe, 2015). Aidha, utamaduni una mchango katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa sababu vipengele vya utamaduni huchangia mjifunzaji kuwa na motisha ya kujifunza lugha lengwa (Gardner, 2005). Katika kubainisha sababu za kuwapa wanafunzi lakabu walimu wengi miongoni mwa waliohojiwa katika utafiti walieleza kuwa wanafunzi wanapewa lakabu za Kiswahili ili kukidhi kipengele cha utamaduni wa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya walimu walieleza kuwa wao huwapa wanafunzi lakabu kama kipengele cha utamaduni kwa sababu kipengele hicho kina mchango katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni kama vile kuwasaidia wanafunzi kuzama kindakindaki katika jamii yenye lugha lengwa. Kwa mfano mtoataarifa mmoja ambaye ni mwalimu alitoa maelezo kama ifuatavyo:

> …..moja ya mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni ni uzamiaji wa kindakindaki. Katika utekelezaji wa mbinu hiyo wanafunzi hukaa katika familia za wenyeji jamii ili waweze kujifunza lugha na utamaduni. Kwa hiyo mimi huwapa wanafunzi hao lakabu ili ziwasaidie kuzama kindakindaki katika jamii ya wenyeji wakati wa ujifunzaji Kiswahili.

MEK ya Robert C. Gardner 2005 katika ya mhimili unaohusu mwingiliano wa tamaduni imesisitiza wajifunzaji wa lugha ya kigeni kuwa na sifa za utamaduni wa lugha wanayojifunza kwa sababu sifa hizo hurahisisha mwingiliano wa wajifunzaji na jamii yenye lugha lengwa. Aidha, kwa mujibu wa modeli hiyo mwingiliano wa tamaduni hurahisisha ujifunzaji wa Lgn na utamaduni wake. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa walimu wanaotumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn wanakubaliana na maelezo ya modeli hiyo katika kurahisisha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn na utamaduni kutokana na kupata nafasi ya kuzama kindakindaki katika jamii ya wazawa wa lugha ya Kiswahili. Hali hiyo inadhihirisha kuwa lakabu kama sehemu ya utamaduni zinawasaidia wanafunzi kuzama kindakindaki katika jamii ya wazungumzaji wazawa wa Kiswahili ili kupata urahisi wa kujifunza Kiswahili. Pia, lakabu hizo zinawasaidia wanafunzi kujifunza vipengele mbalimbali vya utamaduni wa wenyeji.

**Kuepuka Makosa ya Matamshi ya Majina ya Wanafunzi**

Kukosea matamshi ya jina la mwanafunzi kunasababisha wanafunzi kujihisi vibaya na hata kumchukia mwalimu aliyekosea matamshi hayo (Glenz, 2014). Katika usaili uliofanywa ilibainika kuwa matamshi ya majina mengi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama Lgn ni ni magumu. Hali hiyo imekuwa ikiwasababisha walimu hao kukosea matamshi ya majina ya ya wanafunzi ambayo ni magumu. Usaili ho umeonesha kuwa wanafunzi hawapendi matamshi ya majina yao yanapokosewa.

Baadhi ya watoataarifa walifafanua kuwa makosa ya matamshi ya majina ya wanafunzi husababisha changamoto kadhaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa nukuu ifuatayo unaonesha hali hiyo.

> …majina ya wanafunzi wa kigeni ni magumu na wanafunzi wa kigeni wanachukia kukosewa kwa matamshi ya majina yao.…..mwaka 2017 nilikosea kutamka jina la mwanafunzi ambaye aliitwa Keauna, baada ya kipindi alinifuata ofisini kunielekeza namna ya kutamka jina lake. Baadaye aliniambia kuwa alikuwa anajisikia vibaya nilipokuwa ninakosea kutamka jina lake kwa sababu wenzake walimcheka akakosa furaha…. Pia, mimi nilijihisi vibaya.

Matokeo katika nukuu hiyo yanaonesha kuwa kukosea matamshi ya lakabu za wanafunzi kunawafanya wanafunzi wajihisi vibaya. Aidha, walimu nao wanapokosea kutamka majina ya wanafunzi hujihisi vibaya. Hii ni ishara kuwa kukosea kutamka majina ya wanafunzi ni jambo ambalo halikubaliki na ama wanafunzi au walimu.

Pia, ufafanuzi mwingine ulionesha kuwa kukosea matamshi ya majina ya wanafunzi ni jambo ambalo wanafunzi hulihusisha na walimu kutokuwa makini katika ufundishaji au hata kufikiri kuwa walimu hawawapendi wanafunzi waliokosewa majina yao. Aidha, wanafunzi wengine hukosa motisha ya ujifunzaji kwa sababu hiyo. Maelezo hayo yanadhihirika katika nukuu ifuatayo:

> …wenzetu hawapendi kabisa majina yao kukosewa, unajua mwalimu anapokesea kutamka jina la mwanafunzi inaweza kusababisha mwanafunzi akafikiri kuwa mwalimu hampendi au hayuko makini katika ufundishaji. Pia, kunaweza kumwondolea motisha ya ujifunzaji au akamchukia mwalimu na somo lake.

Sambamba na maelezo hayo, mtoataarifa mmoja alieleza kuwa mwalimu anapokosea matamshi ya jina la mwanafunzi hupotosha maana ya jina hilo na wanafunzi hawapendi matamshi ya majina yao yakosewe. Matokeo hayo yanazidi kuonesha kuwa mwalimu anapofanya makosa mengi wakati wa ufundishaji si tu huwasababisha wanafunzi wakose motifha ya ujifunzaji na kuwaona walimu kuwa hawawapendi bali hupotosha maana za majina ya wanafunzi. Hali hiyo in kinyume na maelezo ya wataalamu kama Mensah na Ndimele (2020) ambao waliowahi kueleza kuwa jina la mtu huwa na maana. Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa kukosea matamshi ya majina ya wanafunzi ni kupotosha maana za majina hayo. Hivyo, walimu wanapotumia lakabu za wanafunzi ili kuepuka makosa ya matamshi ya majina ya wanafunzi tafsiri yake ni kuwa walimu wanaepuka upotoshwaji wa maana za majina ya wanafunzi.

Aidha, MEK inaeleza kuwa wanafunzi wanahitaji mazingira mazuri katika ujifunzaji wa Lgn ili waweze kufanikiwa katika ujifunzaji. MEK inaongeza kuwa ufundishaji wa lugha ya kigeni unahitaji walimu wanaomudu mazingira ya ufundishaji wa lugha hiyo. Kwa hiyo, kulingana na maelezo ya modeli hiyo walimu wanaotumia lakabu za wanafunzi ili kuepuka makosa ya matamshi ya majina ya wanafunzi wanachangia katika kuwapa wanafunzi mazingira ya ujifunzaji kwa sababu lakabu zinazotumika ni rahisi kuzitamka hivyo hawakosei matamshi ya majina ya wanafunzi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano iliyobainishwa na watoataarifa Ikionesha majina yenye matamshi magumu na lakabu zilizotumika kuepusha makosa ya matamshi ya majina hayo:

**Jedwali Lenye Mifano ya Majina ya Wanafunzi yenye Matamshi Magumu na Lakabu Zilizotumika Kuepusha Makosa ya Matamshi yake**

| Na. | Jina | Lakabu | Lugha |
|---|---|---|---|
| 01. | Boujour | Simba | Kiswahili |
| 02. | Chealsea | Zawadi | Kiswahili |
| 03. | Curley | Sanaipei | Kimasai |
| 04. | Junwein | Zuena | Kiswahili |
| 05. | Keauna | Bahati | Kiswahili |
| 06. | Kimberley | N'kanfu | Kimeru |
| 07. | Tylor | Tilya | Kimeru |

**Kutekeleza Utaratibu wa Chuo/Taasisi**

Baada ya kuchambua data iliyokusanywa wakati wa usaili, ilibainik kuwa baadhi ya walimu hutumia lakabu kwa sababu tu ya kutimiza utaratibu wa vyuo/ taasisi zao. Walimu hao walieleza kuwa wao hawawapi wanafunzi lakabu, lakini ni utaratibu wa kawaida kuendelea kutumia lakabu za wanafunzi ambazo walipewa kabla na baada ya kufika Tanzania. Ufafanuzi wa walimu hao ulionesha kuwa baadhi ya walimu hutumia lakabu za wanafunzi kwa kuwa wamekuta chuo/taasisi ikiwa na utaratibu huo. Yaani walimu hao wanatumia lakabu za wanafunzi bila kujua sababu na umuhimu wake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn.

**Hitimisho**

Lakabu za wanafunzi ni miongoni mwa mitindo au mikakati inayotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kutokana na sababu mbalimbali. Makala haya yameonesha kuwa sababu za kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn ni pamoja na kuwapa wanafunzi utambulisho, kuweza kuwakumbuka kwa lakabu zao, ugumu wa matamshi ya majina ya wanafunzi, kutumika kama motisha ya ujifunzaji, kukidhi kipengele cha utamaduni na kutekeleza utaratibu wa chuo/taasisi husika. Makala haya yanapendekeza kuendelea kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa sababu zipo sababu mbalimbali za kutumia lakabu za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lgn. Pia, makala haya yanapendekeza kuwa ni muhimu walimu wapewe mafunzo kuhusu matumizi ya lakabu katika ufundishaji na ujifunzaji ili watambue faifda za matumizi hayo katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Vilevile, makala haya yanatoa wito kwa wataalamu wengine kuchunguza madhara ya kutumia lakabu zisizofaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ili waweke bayana maarifa hayo.

**Marejeleo**


Agyekum, K. (2006). The Sociolinguistic of Akan Personal Names. *Nordic Journal of African Studies*, *15*(2), 206-235.

Atolagbe, D., Abegunde, C., & Morofonfoye, O. (2015). Generation and Attribution of Nicknames among Secondary School Students: Indices of Linguistic Creativity. *Research on Humanities and Social Sciences*, *5*(20), 104-109.

Bobrova, M. (2022). Nicknames in Teaching Russian as a Foreign Language. *Russian Language Studies*, *20*(1), 22-34. Inapatikana katika DOI 10.22363/2618-8163-2022-20-1-22-34.

Diao, W. (2014). Between Ethnic and English Names: Name Choice for Transnational Chinese Students in a US Academic Community. *Journal of International Students*, *4*(3), 205-222. Inapatikana katika http://jistudents.org.

Filani na Melefa (2014). A Socio-Semiotic Study of Nicknaming among Undergraduates katika Chuo Kikuu cha Naijeria. *Linguistik Online*, *68*(6), 22-42. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.13092/lo.68.1632.

Garayeva, A. K., Akhmetzyanov, I. G., & Khismatullina, L. G. (2016). The Significance of Learning Nicknames fo Public Figures in Modern English and American Language Models of the World. *International Journal of Environmental and Science Education*, *11*(4), 10337-10345.

Gardener, R. C., & Macltyre, P. C. (1993). A Student's Contributions to Second Language Learning. Part II: Affective Variables. *Language Teaching*, *26*, 1-11. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.1017/S0261444800000045.

Gardner, C. R. (2000). Correlation, Causation, Motivation and Second Language Acquisition. *Canadian Psychology*, *41*, 1-24. http://dx.doi.org/10.1037/h0086854.

Gardner, R. C. (1985). *Social Psychology and Second Language Learning: The Role of Attitudes na Motivation*. London: Edward Arnold Publishers.

Glenz, T. (2014). The Importance of Knowing Students' Names. *Journal on Best Teaching Practice,* 21-22.

Jamalvandi, B., & Jamalvandi, A. (2016). Application of Nicknames among Ilami Kurdish Students, West of Iran. *ResearchGate/Sociology Study*?, *6*(9), 604-614. Inapatikana katika doi:10.17265/2159-5526/2016.09.006.

Kennedy na Zamuner. (2006). Nicknames and the Lexicon of Sports. *American Speech*, *81*(4), 387- 422.

Koehn, S. C. (2015). Use of Self-selected Nicknames by Female Kuwaiti Students and their Perception of the Impact of Nicknames up on their Learning in the Classroom. *Near and Middle Eastern Journal of Research in Education*. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.5339/nmejre.2015.2.

Kuranchie, A. (2012). Student's Nicknames: Their Source and Effects on Learning. *Journal of Education and Practice*, *3*(14), 23- 41.

Lakaw, A. (2006). *Hiding Behind Nicknames: A Linguistc Study of Anonymity in IRC Chatrooms*. Student Thesis. Vaxjo University. Inapatikana katika http://Inu.diva-portal.org/smash/record.jsf?pid=diva2:206935.

Mapunda, G. (2014). What Do My Students Call Me? Nicknaming of Lecturers by Students at the University of Dar es Salaam. *Journal of Linguistics and Language in Education*, *8*(1), 90-107.

Mensah, E. O., & Ndimele, R. I. (2020). King Shumba, Smilling Devil and Baby Doctor: A Sociolinguistic Study of Lecturers' Nicknames in Two Nigerian Universities. *African Identities*. Inapatikana katika DOL: 10. 1080/14725843.2020.1813544.

Mphande, L. (2006). Naming and Linguistic Africanism in African American Culture. In Mugane, J. P. (Ed.), *Selected Proceedings of the 35th Annual Conference on African Linguistics*ed (104-113). Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project.

Oxford, R. (2003). *Language Learning Style and Strategies*. USA: Cambridge University Press.

Reyes, M., & Rodriguez, J. (2006). *Teaching English in Mixed-ability Classrooms: Some Teachers' Thoughts on Responding to the Needs of all Learners*. Inapatikana katika www.teaching.english.org.uk.

Saleh, F. H. (2019). *Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Darasa Mseto la Wingilugha*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wazungumzaji wa Lugha Nyingine (M.Ed.TEKSOL) Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Sobane, K. (2016). The Pragmatics of Nicknames Students Use for their Lecturers. Inapatikana katika *https://www.researchgate.net/publication/292149459*.

Starks, D., & Taylor-Leech, K. (2021). A Research Project on Nicknames and Adolescent Identities. *New Zealand Studies in Applied Linguistics*, *17*(2), 87-97.

Wa'Njogu. (2008). Ufundishaji wa Kiswahili Marekani: Maendeleo na Changamoto. *Swahili Forum*, *15*, 121-133.

Xinran, W. (2023). Stories of Names: Exploring Chines High School Language-other-than-English Learners' Foreign Name(s) Usage and its Role in Multilingual Identity Construction. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 1-15. Inapatikana katika DOI: 10,1080/01434632.2023,2170392.

Yi, Q. (2010). Culture Understanding in Foreign Language Teaching. *Canadian Centre of Science and Education*, *3*(4), 58-61.

Yule, G. (2010). *The Study of Language*. United Kingdom: Cambridge University Press.